# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE

**7 SEPTEMBA, 2018**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**KIKAO CHA NNE – TAREHE 7 SEPTEMBA, 2018**

## I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Najma Murtaza Giga (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

**MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Athuman Hussein
2. Ndg. Neema Msangi
3. Ndg. Yona Kirumbi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wafuatao waliwasilisha Mezani hati zifuatazo:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), Bill, 2018].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA :**

Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), Bill, 2018].*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2), Bill, 2018].*

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 40: Mhe. Flatei Gregory Massay

Nyongeza: Mhe. Flatei Gregory Massay

### OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Swali Na. 41: Mhe. Maryam Salum Msabaha (kwa niaba yake Mhe. Cecilia Daniel Paresso)

Nyongeza: Mhe. Cecilia Daniel Paresso
Mhe. Joseph Roman Selasini
Mhe. Mwanne Ismail Mchemba
Mhe. Richard Mganga Ndassa

### WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Swali Na. 42: Mhe. Fakharia Shomar Khamis

Nyongeza: Mhe. Fakharia Shomar Khamis
Mhe. Alex Raphael Gashaza
Mhe. Maryam Salum Msabaha

### WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na. 43: Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala

Nyongeza: Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala
Mhe. Mohamed Juma Khatib
Mhe. Hashim Ayubu Jaku
Mhe. Zakharia Paulo Issaay

Swali Na. 44: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

Nyongeza: Mhe. Fredy Atupele Mwakibete

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 45: Mhe. David Ernest Silinde

Nyongeza: Mhe. David Ernest Silinde
Mhe. Dkt. Immaculate Semesi Sware
Mhe. Mary Michael Nagu

Swali Na. 46: Mhe. Ally Seif Ungando

Nyongeza: Mhe. Ally Seif Ungando

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 47: Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi (kwa niaba yake Mhe. Juma Othman Hija)

Nyongeza: Mhe. Juma Othman Hija
Mhe. Saada Salum Mkuya
Mhe. Shally Josepha Raymond
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili

Swali Na. 48: Mhe. Amina Saleh Mollel (kwa niaba yake Mhe. Hawa Mchafu Chakoma)

Nyongeza: Mhe. Hawa Mchafu Chakoma
Mhe. Khadija Nassir Ali
Mhe. Susan Anselm Lyimo

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na. 49: Mhe. Mgeni Jadi Kadika (kwa niaba yake Mhe. Juma Kombo Omar)

Nyongeza: Mhe. Juma Kombo Omar
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto

**WIZARA YA KILIMO:**

Swali Na. 50: Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla

Nyongeza: Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla

**WIZARA YA MADINI:**

Swali Na. 51: Mhe. Musukuma Joseph Kasheku (kwa niaba yake Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba)

Nyongeza: Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba

Swali Na. 52: Mhe. Janet Zebedayo Mbene

Nyongeza: Mhe. Janet Zebedayo Mbene

**MATANGAZO:**

1. Wageni wa Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi – OWM ambao ni:-

   (a) Mhe. Mihayo Juma N'hunga – NW-OMPR-SMZ
   (b) Ndg. Shaaban Mohamed – KM, OMPR – SMZ

2. Wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge wafuatao walitambulishwa:-

   (a) Mhe. Elias John Kwandikwa
   (b) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka
   (c) Mhe. Alex Rapahel Gashaza

3. Wanafunzi 66 na Walimu 11 kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Holly Trinity ya Dodoma.

**MASUALA YANAYOHUSU UTARATIBU:**

1. Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma akitumia Kanuni 68(7) alidai kwamba wakati akiingia katika Viwanja vya Bunge alipokea taarifa kwamba Mkuu wa Wilaya ya Chemba amewafukuza Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wa Chama cha Wananchi (CUF) katika Wilaya ya Chemba. Aidha, alihoji iwapo hatua hiyo ya Mkuu wa Wilaya ndio kazi aliyotumwa na Rais kwa kuwa amekuwa na tabia hiyo.

   Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Najma Murtaza Giga alitoa Mwongozo wake kwa kusema kwamba jambo hilo ndio analisikia kwa mara ya kwanza kwa Mbunge huyo na hivyo basi, Serikali imelisikia na ilifanyie kazi na kutoa taarifa.

2. Mhe. George Malima Lubeleje akitumia Kanuni 68 (7) aliomba Mwongozo kuhusiana na Majibu ya Swali Na. 43 ambapo alihoji kwamba iwapo Viwanda kama cha Kagera Sugar vimezalisha Sukari ya kutosha lakini bado bei iko juu kwa sababu kuna uingizwaji wa sukari nchini kinyume na taratibu na kwamba Serikali inachunguza hali hiyo kwa kuwa kuna masuala ya jinai ndani yake. Je, bei iendelee kupanda mpaka uchunguzi huo ukamilike?

   Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Najma Murtaza Giga alitoa Mwongozo wake kwa kuitaka Serikali hapo baadae leo ije na taarifa kuhusu namna ya kukabiliana na ongezeko hilo la bei.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2018].*

1. Waziri wa Katiba na Sheria alisoma Hotuba kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018.
2. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria alisoma Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huo.
3. Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani alisoma maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huo.

Wabunge wafuatao walipata fursa ya kutoa mchango wao kuhusu Muswada husika:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Salome Wycliffe Makamba | - | CHADEMA |
| 2. | Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | - | CCM |
| 3. | Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro | - | CCM |
| 4. | Mhe. Abdallah Ally Mtolea | - | CUF |
| 5. | Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi | - | AG |
| 6. | Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi | - | W/Katiba |

## V. KUHITIMISHA HOJA:

Mtoa Hoja, Waziri wa Katiba na Sheria akitanguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alihitimisha Hoja yake kwa kutoa ufafanuzi na kujibu maswali mbalimbali yaliyojitokeza katika mjadala na michango ya Wabunge.

## VI. KAMATI YA BUNGE ZIMA

Baada ya Mwenyekiti wa Bunge kuongeza muda kabla ya kuahirisha Kikao, Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2018 na kupitisha Ibara kwa Ibara ambapo Ibara zote ziliafikiwa pamoja na marekebisho yake.

## VII. TAARIFA YA MTOA HOJA

Mtoa Hoja alitoa Taarifa kuwa Bunge limepitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2018.

## MUSWADA HAUKUSOMWA KWA MARA YA TATU

## VIII. BUNGE KUSITISHWA:

Saa 7:24 mchana, Mhe. Najma Murtaza Giga (Mwenyekiti) alisitisha Bunge mpaka Jumatatu tarehe 10 Septemba, 2018 saa 3:00 asubuhi.